**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# TAARIFA KWA UMMA

**Dodoma, Novemba 08, 2025**

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inapenda kuutaarifu umma kuwa, kwa mujibu wa kalenda ya kitaaluma ya mwaka wa masomo 2025/2026, vyuo vyote vya elimu ya kati na juu, vya umma na binafsi, vitafunguliwa kama ifuatavyo:

**Wanafunzi wa mwaka wa kwanza** wanatakiwa kufika vyuoni kuanza programu ya utangulizi (orientation programme) kuanzia tarehe **17 Novemba 2025,** kabla ya kuanza rasmi masomo.

**Wanafunzi wanaoendelea** watarejea vyuoni kuanza rasmi masomo kuanzia tarehe **24 Novemba 2025.**

Aidha, Wizara inawahimiza wanafunzi wote kufika vyuoni kwa wakati, kufuata ratiba zilizopangwa, na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kitaaluma. Tunawatakia masomo mema.

Imetolewa na:
Katibu Mkuu
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

#ElimunaUjuziMpangoMzima
www-moe-go-tz